
# UTANGULIZI

- Mradi unaotafiti kiwango cha kukabiliana na hali katika sehemu zilizo nusu kame umechunguza ni nini kinachowafanya watu kuwa katika hali ya hatari na madhara yanayohusiana na mabadaliko ya hali ya hewa katika sehemu zilizo kame kwenye bara la Africa na Asia.





- **Kama sehemu ya Mradi huu, muungano kati ya chuo kikuu cha Nairobi, Kenya, Chuo kikuu cha Addis Ababa, Ethopia na chuo kikuu cha Anglia Mashariki, na shirika la Oxfam Uingereza, wamekuwa wakifanya kazi katika nchi ya Kenya na Ethopia kwa miaka minne iliyopita.**

- Kwa kuongea na watu kama wafugaji na wakulima ambao maisha na ustawi wao umetegemea mazingira, tulitumaini kutambua mambo yatakayofanya kukabiliana na hali ya ulimwengu unaobadiliki kuwa rahisi.





- **Muonyesho huu unanuiwa kusaidia kupeana majibu ambayo tumepokea kufikia sasa, kusambaza maoni na maarifa ambayo yatafanya jamii, mashirika ya ndani na serikali ya Kenya, kukabiliana vyema na mabadiliko ya hali ya hewa kutumia njia ambazo zitalinda na kuboresha maisha ya watu katika siku za usoni.**

- Katika taifa la Kenya, tumefanya kazi sana kwenye Kaunti za Isiolo na Meru ambako nchi inaendelea kuwa kame. Katika miaka hiyo minne tuliyokuwa tukifanya utafiti huu, tumeongea na watu 1,023 katika jamii 10 kutoka Kaunti hizi mbili. Pia tumeongea na washikadau 143 kutoka wadi na pia kitaifa.

- **Tunaelewa kuwa:**

  - Watu wanatofautiana katika hali ya kuathirika au uwezo wa kukabiliana na janga hili

  - Watu wanahaki sio ya kulinda maisha yao tu lakini pia kuwa na sauti ya kuamua ni vipi wanavyoweza kumudu matatizo

  - Kabla ya kuwasilisha suluhu za ukabilianaji, ni lazima kwanza tuelewe ni nini kinasaidia au kuzuia nafasi ya kufaulu na kupitishwa kwa usawa





- Sehemu nyingine za muonyesho huu zinaangazia ujumbe muhimu kutoka kwa kazi yetu kwa ufupi.

# MADA 1:
# HALI YA HEWA, MAJI NA MAISHA

- **Maeneo kame Africa Mashariki yanaathirika kutokana na mbadliko ya hewa:**

  - Joto wastani linaendelea kuongezeka na maongezeko haya yako juu zaidi katika sehemu kame ulimwenguni.

  - Huenda kukawa na mabadiliko katika muundo wa mvua, kuendelea kufanya makadirio ya hali ya hewa kuwa magumu.

  - Sehemu hii inaweza athirika na hali ya hewa iliyokithiri, kuongezea ukame na mafuriko.





- **Hii inaweza maanisha kuwa viwango vya maji kwenye udongo na mito huenda vikawa si vyakutegemea, na basi:**

  - Kuathiri malisho, mimea na mifugo.

  - Kuleta mabadiliko kwenye mazingira- uwezekano wa kuongeza mabadiliko katika aina ya mimea na miti inayokua katika nchi.

- **Lakini utafiti wa 'ASSAR' unasisitiza kuwa mabadiliko ya hali ya hewa hayawezi zingatiwa pekee- hii ni sehemu ya muungano wa mambo mengi kwenye mtandao.**

  - Kwa mfano, athari ya ukame haisababishwi na hali ya hewa peke yake lakini na mambo mengine pia kama jinsi nchi inavyotumika na mabadiliko ya watu kupata malisho na maji.

- **Hii inamaanisha kuwa, katika kuelewa vyema athari za mabadiliko ya hali ya hewa na majibu ya watu kuhusiana na mabadiliko ya mazingira, inabidi tuwe na taswira kamili ya changamoto wanazokumbana nazo katika maisha.**

- **Jinsi mbali mbali yanatumiwa na jamii kukabiliana na mabadiliko ya hali ya hewa ni kama:**


  - Kutoa njia za mseto za kutafuta riziki kwenye maisha

  - Kubadilisha mifugo au aina ya mimea

  - Kuhamia sehemu nyingine kutafuta kazi

  - Kujenga mifumo ya msaada ya kijamii

  - Kuboresha jinsi ya kutunza rasilimali za asili



- **Kuna mambo tofauti yanayoshawishi mafanikio ya haya, na yanalingana na jinsia ama umri wa watu na tabia nyingine za kijamii.**

- **Kujibu maswala haya yanahitaji shirika tofauti, sehemu na ngazi mbali mbali kwenye serikali kufanya kazi pamoja. Kwa mfano, ni:**

  - Kusaidia makundi tofauti ya wafugaji kubadilisha nchi kwa kupunguza kushindana kwa rasilmali

  - Kuhakikisha maji yanapatikana kwa watumizi na kwa matumizi yote kwa hiyo mahali.





# MADA 2: KUISHI NA MABADILIKO



- **Maswali ya utafiti wa ASSAR unauliza: Ni vipi wanaume na wanawake (wa makundi tofauti na umri) Isiolo na Meru wanafanya mabadiliko nyumbani mwao jinsi wanavyojikinga na athari na kukabiliana vyema na mazingira yanayobadilika:**

- **Tuligundua kwamba wafugaji kutoka jamii ya waborana wanafanya mambo matatu makuu katika kukabiliana na mabadiliko ya hali ya hewa:**

  - Kuongeza shughuli za ufugaji au uhamiaji ili kujikinga na umaskini unaosababishwa na mabaidiliko ya hali ya hewa.

  - Kubadilisha kutoka ufugaji na kufanya ukulima-ufugaji, biashara, kazi rasmi na zisizokuwa rasmi.

  - Wanawake kuendelea kujihusisha na biashara ndogo ndogo, zingine ambazo zaweza kuhatarisha maisha yao.





- **Wanawake na wanaume wanaathirika tofautu jinsi ilivyo kwa wazee na watu wa umri mdogo. Vijana huona vigumu kutimiza matumaini na ndoto zao hasa katika sehemu za mijini.**

- **Kuingia katika shughuli mpya inamaanisha maamuzi magumu. Mara nyingine jamii zinatawanyika kuenda sehemu tofauti. Inaweza kuwa vigumu kuingia kwenye shughuli ambazo hazitegemei hali ya hewa, na sio watu wote wako tayari kuhama.**

- **Kutoweza kuhama wakati waukame inaweza kuathiri vibaya watu hasa wanawake na wazee.**

- **Watu wanaathirika zaidi wakati majanga yanapotokea moja baada ya lingine kiasi cha kufanya vigumu kurudi kwa hali ya kawaida ya maisha.**

- **Usaidizi zaidi unatakikana kuongeza nafasi za kazi zisizotegemea maliasili ama zisiathirika na hali ya anga ama hewa. Hii itasaidia kujenga uwezo wa watu katika kukabiliana na kuwa imara kwenye mabadiliko yanayoendelea ulimwenguni.**

- **Hatua muhimu za kuchukua mbali na ufugaji na ukulima ni:**

  - Kutoa fursa na mafunzo ya ujuzi unaolingana na hali kamili katika soko la kazi

  - Kutoa nafasi ya upatikanaji rahisi wa mikopo, mali anzilishi, mafunzo na ushauri wa kuanzisha biashara ndogo ndogo.

  - Kuhakikisha kunaupatikanaji wa huduma muhimu kama maji safi kwa urahisi, na huduma za afya kwa watoto.

- **Kwa wale wanaondelea kutegemea ufugaji na ukulima, wanahitaji msaada kufanya:**

  - Kuongeza upatikanaji wa aina ya mifugo inayostahimili ukame ama aina ya mimea unayoiva haraka wakati mvua inapopatikana.

  - Kupata bima ya ukulima na ufundi rahisi wa kuhifadhi maji kama unyunyizaji maji wa matone na kutega maji ya mvua.

- **Kuongeza ustahimilivu kwa wote, ni lazima:**

  - Tuboreshe huduma muhimu kama maji, afya, na pia afya ya wamama.

  - Tuimarishe mipango zalishi ya usalama wa kijamii ili kusaidia jamii nyingi kupata afueni kutokana na athari na majanga ya mazingira.



- **Kupitia kwa kazi yetu tunatumaini kusaidia watu kwa:**

  - Kufanya kazi na watunga sera ili kuwasaidia kuelewa jinsi watu wanavyoishi na mabadiliko, jinsi mabadiliko yanavyoathiri watu tofauti na mambo ambayo watu, hasa wanawake na watu walio na mazingira magumu zaidi, wanapaswa kuweza kutatua

  - Kusaidia jamii kupitia mafunzo, kama vile, kukabiliana na masuala ya upungufu wa malisho kupitia shughuli za kujenga uwezo.

  - Kufanya utafiti zaidi, kama vile, juu ya ustawi, matarajio ya vijana, uhamiaji



# MADA 3: KUSIMAMIA MABADILIKO



- **Kuhakikisha kuwa kila mtu anaweza kupata rasilimali wanazohitaji inahitaji uratibu katika sekta mbalimbali na viwango vya serikali, lakini pia inahitaji ushiriki wa watu wanaoishi na kufanya kazi katika maeneo ya kavu ili waweze kuelezea nini wanataka na jinsi wanavyotaka ifanyike.**

- **Utafiti wa ASSAR unaonyesha umuhimu wa taasisi kufanya kazi pamoja kanda na kitaifa, na pia kutambua ujuzi na maarifa wa jamii. Hii itasaidia kusimamia matatizo magumu kama vile:**

  - Kusimamia vizuri matumizi ya maji kutoka kwa mto Ewaso N'giro North inayopitia eneo hilo

  - Mabadiliko katika upatikanaji wa malisho yanayoletwa kwa njia tofauti za matumizi ya ardhi. Kwa mfano, hifadhi wa wanyamapori katika Jimbo la Isiolo na sehemu jirani inaongezaka, na kuleta mabadiliko katika utawala wa rasilimali, hasa ndani ya maeneo ya hifadhi.

  - Kupunguza hatari kutokana na ukame - wafugaji wengi katika Isiolo na Meru wametuambia kuwa wamelazimika kusafiri zaidi na ng'ombe zao, na kuongeza muda wao kuwa mbali na familia zao.

  - Kutatua migogoro - kwa sababu ya upungufu wa upatikanaji wa malisho na maji, wafugaji wanakuwa na mgogoro mkubwa na wachungaji wengine wakati wanapohamai mbali na maeneo yao, na wakulima na wanachama wa hifadhi, hasa katika wakati wa ukame.

- **Jitihada kubwa zinafanyika kushughulikia matatizo ya usimamizi wa rasilimali kwa mtazamo wa mabadiliko ya hali ya hewa, lakini changamoto muhimu zipo:**

  - Mpangilio wa usimamizi wa rasilimali mara nyingi unatokea kwa uratibu mdogo kati ya mashirika na watu, na bila kuhusisha jamii.

  - Mipango ya usimamizi wa rasilimali inayolenga matatizo tu (kama vile katika kusimamia matatizo ya maji na ukame) badala ya mpango wa kuangalia mbele.

  - Sauti za jamii hauzingatiwi wakati wa kubuni mipango wa miradi.

  - Ukosefu wa mipangilio ya matumizi ya ardhi na usimamizi wa rasilimali katika eneo hilo kunaweza kusababisha matatizo zaidi, kwa mfano kati ya wanachama wa hifadhi na wale ambao sio wanachama.

  - Kuwepo kwa mifugo na wanyamapori sehemu moja kunaweza kusababisha migogoro zaidi kati ya watu na wanyamapori. Jamii nyingine huhisi kwamba wanyamapori ni muhimu zaidi kuliko wao.





- **Kupitia kazi yetu tunatarajia kuunga mkono hatua za serikali kwa njia zifuatazo:**

  - Kufanya kazi na watunga sera katika ngazi za mitaa, kata na kitaifa ili kukuza njia bora za kufanya kazi pamoja juu ya mipango ya usimamizi wa rasilimali.

  - Kuboresha mipangilio ya taasisi iliyopo ili kuratibu usimamizi wa rasilimali na kupunguza hatari kwa kuonyesha mazoezi ya sasa mazuri (kama vile kamati za kata za kuendesha mipango dhidi ya mabadiliko ya hali ya hewa, na kamati ya uendeshaji wa kata inayoongozwa na Mamlaka ya Usimamizi wa Ukame (NDMA)

  - Kusaidia ushirikiano bora wa ushirika na taasisi za jadi.

  - Kuthamini ujuzi wa watu juu ya mazingira yao na kuwashirikisha katika maamuzi, hasa wanawake na vijana

  - Kusaidia juhudi za serikali ya kata kutambua taasisi za kimila (kama vile kamati za Dedha katika usimamizi wa malisho na maji)

  - Kuzingatia hasa juu ya kushauri serikali ya kata juu ya ushirikiano na ushiriki (kama vile kufanya mashauriano ya umma kwa lazima katika kuandaa Mpango wa Maendeleo ya Kata ya miaka 5).







# MADA 4: KUZINGATIA UHABA WA MALISHO



- **Baadhi ya changamoto kuu za wafugaji katika eneo hili ni matatizo yanayohusiana na uhaba wa malisho.**

**Katika utafiti wetu, tulizingatia kuelewa tatizo la uhaba wa malisho na ufumbuzi wake, ikiwa ni pamoja na kupata mtazamo tofauti juu ya njia bora za kukuza usimamizi bora wa maeneo ya malisho.**

- Uzalishaji wa mifugo hutegemea malisho ya asili ambayo haipatikani kwa usawa katika nafasi na wakati - uhamiaji huwasaidia wafugaji kupata na kutumia rasilimali hizi.

- Katika kata ya Isiolo, fursa ya kutumia malisho hutegemea taasisi za kimila kama dedha na njia nyingine za kusimamia ardhi kama vile hifadhi wa wanyamapori.

- Katika nyakati za hivi karibuni upatikanaji wa maji ndani ya Jimbo la Isiolo umeshuka, kumekuwa na mabadiliko ya taratibu katika utungaji wa mimea na ushindani mkubwa wa malisho kutoka kwa jamii jirani

- Changamoto zingine pia zipo kama vile kutokuwa na taratibu wa kuzuia magonjwa ya mifugo

- **Wakati wa mradi wa ASSAR tulijadili njia mbalimbali za kukabiliana na tatizo la uhaba wa malisho kama vile kuwa na hifadhi wa wanyamapori, kubinafsisha na kufunga mashamba, kuunga mkono dedha na njia nyingine za jadi za usimamizi wa rasilimali, na kuwasaidia watu kubadili maisha yao ili wasitegemee ufugaji pekee.**

**Watu wa Kinna, Kulamawe na Kachuru na wakilishi kutoka kwa serikali na mashirika yasiyo ya kiserikali ambao tulizungumza nao walipendelea kwa jumla mbinu mbili za kukabiliana na uhaba wa malisho.**


- Kufunga mashamba na kubadilisha muundo wa mifugo kwa kufuga ngamia na mbuzi badala ya ng'ombe na kondoo, ilikuwa ya kupendezwa zaidi katika jamii tatu ambazo tumefanya kazi nao na wakilishi kutoka kwa serikali na mashirika yasiyo ya kiserikali

- Kubadilisha muundo wa mifugo kulipendwa zaidi na wanawake kuliko wanaume.

- Katika Kinna na Kachuru, chaguo la kuwasaidia jamii kugeuka na kutekeleza shughuli nyingine za maisha kando na ufugaji ulipendekezwa zaidi.







- **Kutoka kwenye majadiliano tuliyo nayo na watu tunadhani kuwa njia yoyote ya kukuza usimamizi wa nchi endelevu lazima ijumuishe:**

- Njia bora za watu kushauriana juu ya upatikanaji wa rasilimali na habari kuhusu mambo kama utabiri wa hali ya hewa, hali ya malisho na maendeleo ya miundombinu

- Usaidizi zaidi ili kuwezesha jamii ikiwa ni pamoja na wanawake na vijana kufanya kazi kwa pamoja, kupata huduma, na kusajili ardhi yao

- Uboreshaji wa mambo kama fursa ya ajira, mikopo na masoko kusaidia watu kushiriki kwa aina tofauti za shughuli za maisha


- Huduma za uenezi bora ili kusaidia kwa kushughulikia aina mpya ya mifugo na habari juu ya mbinu tofauti za ufugaji wa wanyama

- **Kupitia kazi yetu tunatarajia kusaidia usimamizi wa maeneo ya malisho endelevu kwa njia zifuatazo:**

- Kusaidia jamii kwa kutoa mafunzo juu ya njia za kusimamia malisho na kuongeza maarifa kuhusu ufugaji wa ngamia

- Kusaidia mashauriano kati ya watumiaji wa maeneo ya malisho ili kukuza ushirikiano bora

- Kutoa taarifa ili kusaidia kuboresha sharia za ngazi ya kata, sera, na mipango ya kukuza usawa katika utumiaji wa rasilimali



UEA University of East Anglia · Addis Ababa University · University of Nairobi · OXFAM · ASSAR · CARIAA